



STRENGTHENING FINANCIAL SECTOR RESILIENCE IN CHALLENGING ECONOMIC TIMES

PROCEEDINGS OF THE 21ST CONFERENCE OF
FINANCIAL INSTITUTIONS HELD AT ARUSHA
INTERNATIONAL CONFERENCE CENTRE,
RUSHA

7TH – 8TH MARCH 2024





BANK OF TANZANIA

**STRENGTHENING FINANCIAL SECTOR RESILIENCE
IN CHALLENGING ECONOMIC TIMES**

**PROCEEDINGS OF THE 21ST CONFERENCE OF
FINANCIAL INSTITUTIONS HELD AT ARUSHA
INTERNATIONAL CONFERENCE CENTRE,
ARUSHA**

7TH – 8TH MARCH 2024

@ Bank of Tanzania 2024

For any inquiries on this publication, please contact
Director of Economic Research and Policy,
Bank of Tanzania,
2 Mirambo Street 11884, Dar es Salaam
Telephone: +255 22 223 3328/9
Email: botcommunications@bot.go.tz



Foreword



We are delighted to share the highlights from the 21st Conference of Financial Institutions (COFI), which took place on 7th and 8th March, 2024 in Arusha, Tanzania. The event was co-hosted by the Bank of Tanzania (BOT) and the Tanzania Bankers Association (TBA), and served as an exemplary platform for fruitful engagement and the exchange of ideas pertinent to the financial sector and the broader economy. The theme **“Strengthening Financial Sector Resilience in Challenging Economic Times”** underscored the importance of fortifying the financial industry amidst economic uncertainties. Discussions revolved around three sub-themes: Financial Institution’s Efficiency and Survival in Times of Crisis, Financial Sector Stability in the Wake of Economic Crises, and Technological Innovations in the Delivery of Financial Services - A Catalyst for Resilience. Esteemed resource persons from Tanzania and abroad delivered insightful presentations, fostering robust discussions among distinguished guests, industry leaders, and financial sector experts.

His Excellency Dr. Isidor Philip Mpango, the Vice President of the United Republic of Tanzania, officiated the event and launched the Tanzania Instant Payment System (TIPS) - a groundbreaking initiative aimed at increasing the efficiency of the payment systems in the country. Acknowledging the challenges posed by recent global economic shocks, the Vice President and attendees underscored the need to reinforce the resilience of Tanzania’s financial sector. Esteemed experts highlighted the significance of regulatory frameworks, innovative practices, and technological advancements in promoting stability and efficiency within financial institutions. Strategies for bolstering financial sector resilience during crises, including robust risk management and the adoption of transformative technologies, were thoroughly explored. The conference emphasized the role of the financial sector in navigating economic uncertainties and fostering sustainable growth. It also stressed collaboration among stakeholders to address emerging challenges and promote stability during turbulent times.

As we present the proceedings of the 21st COFI in this book, we earnestly hope that it will serve as a valuable resource in addressing the challenges facing the financial sector and the economy.

**Emmanuel Tutuba
GOVERNOR
BANK OF TANZANIA**



Acknowledgement

We are grateful to the Bank of Tanzania Executive Office, led by Governor Emmanuel M. Tutuba, along with Deputy Governors: Yamungu Kayandabila, Julian Banzi, and Sauda Msemo, for their invaluable guidance and support in the successful preparation of the 21st Conference of Financial Institutions (COFI). We also extend our gratitude to the Tanzania Bankers Association (TBA) for co-hosting the event. Furthermore, we extend our heartfelt thanks to the dedicated members of the technical bench, including Suleiman Missango, Kened Nyoni, Deogratius Macha, Nicholaus Kessy, Lusajo Mwankemwa, Happiness Naumanga, Elias Makoye, Betrida Wilfred, and Tusekelege Joune, who generously devoted their time and expertise to the creation of this booklet. We also express our appreciation to the conference rapporteurs, namely Lorah Madete, Hosanna Mpango, David Kijazi, Aristedes Mrema, Paschal Marubili and Charles Masenya, for their diligent efforts in capturing the proceedings of the conference. Last but not least, our deepest gratitude goes to the resource persons and participants for their willingness to share their wealth of experience and knowledge and for their invaluable contributions to the conference discussions, which have greatly enriched the content of this booklet.



Contents

Foreword	i
Acknowledgement	ii
1.0 OPENING CEREMONY	1
1.1 Sala	1
1.2 Salamu za Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Mhe. Emmanuela Kaganda, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha	1
1.3 Salamu kutoka kwa Bw. Theobald Sabi, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mabenki Tanzania	3
1.4 Maneno ya Utangulizi kutoka kwa Bw. Emmanuel Tutuba, Gavana, Benki Kuu ya Tanzania	5
1.5 Salamu za Ukaribisho kutoka kwa Mhe. Hamad H. Chande, Naibu Waziri wa Fedha	10
1.6 Hotuba ya Ufunguzi ya Mgeni Rasmi, Mhe. Dkt. Philip I. Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania	13
2.0 SUMMARY OF PRESENTATIONS AND DISCUSSIONS	20
2.1 Session One: Financial Institution's Efficiency and Survival in Times of Crises	20
2.2 Session Two: Financial Sector Stability in the Wake of Economic Crises, Regulations, Innovations and Risks Management	25
2.3 Session Three: Technological Innovations in the Delivery of Financial Services: A Catalyst for Resilience	31
3.0 CLOSING	37
3.1 Remarks by Dr. Yamungu Kayandabila, Deputy Governor Bank of Tanzania ..	37



1.0 OPENING CEREMONY

1.1 Sala

Baraza la Maaskofu Tanzania (Askofu Isaac Amani)

Mungu Baba Mwenyezi, Muumba wa ulimwengu wote na Baba yetu, uchumi ni sehemu muhimu sana ya maendeleo ya mwanadamu. Tunakushukuru kwa raia wetu ambaao ndio utajiri wa kwanza wa taifa letu. Tunakushukuru kwa viongozi wetu wa ngazi mbalimbali, wanaotuongoza katika maadili na mafanikio ya maisha yetu.

Tunakushukuru kwa fursa zilizopo kupitia maliasili, wataalamu wetu na wawekezaji wote nchini. Kupitia mkutano huu, tunakuomba utuwezeshe kufanya kazi pamoja kwa malengo ya kujenga taifa letu, tupate maisha bora zaidi kiuchumi, kijamii na wote tushirikiane katika kutafuta na kushiriki matunda ya maendeleo kwa haki. Tunaomba hayo kwako wewe unayeishi na kutawala milele na milele. Amina.

Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (Sheikh Shaban Juma)

Tunaomba hekima itumike katika kikao hiki kwa maslahi ya nchi yetu. Uwasamehe madhambi yao wote walio mbele ya haki na sisi utuonyeshe kuyaepuka madhambi kwa sababu madhambi yanaweza kuzuia neema za Mungu kwetu. Mwongoze Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan na wenzake wote kwa ujumla ili jambo hili la nchi yetu lisimame kama tunavyokusudia. Mungu tunaomba utujalie karama zilizomo katika mioyo yetu zote zitoke kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu. Ee! Mungu tukubalie. Amin.

1.2 Salamu za Mkoa kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Mhe. Emmanuela Kaganda, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha

Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Viongozi wote wa Meza Kuu;

Itifaki imezingatiwa.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, ninaomba niruhusu niweze kuleta mbele yako salamu za Mkoa wa Arusha kwa niaba ya Mkuu wetu wa Mkoa wa Arusha, Mhe. John Mongella.

Kwanza kabisa, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema iliyotuwezesha kukutana hapa leo, kwenye mkutano huu wetu muhimu ambaao umeandaliwa na Benki Kuu pamoja na Jumuiya ya Umoja wa Mabenki nchini.



Pia, ninaomba kutumia fursa hii, kwa niaba ya wananchi wote wa mkoa wa Arusha, kukukaribisha wewe na wageni wote hapa mkoani kwetu. Wananchi wa mkoa wa Arusha wana imani kubwa sana na Serikali yao inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kutokana na kazi kubwa inayofanywa na inayoendelea kufanywa katika kuleta maendeleo kwa wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, kipekee kabisa nichukue fursa hii kukushukuru sana wewe binafsi kwa kukubali mwaliko wa kuja kufungua mukutano huu pamoja na majukumu mengi uliyonayo. Umeupa mukutano huu kipaumbele na kuweza kuja kushirikiana nasi, tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, pia, ninapenda kuchukua fursa hii, kuwashukuru sana waandaaji wa mukutano huu, kwa kutupa heshima kubwa sisi wananchi wa mkoa wa Arusha kwa kutupa nafasi hii ya kuwa wenyeji wa mukutano huu muhimu sana kwenye sekta ya fedha na uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, tunafahamu kabisa sekta ya fedha ni muhimu sana, na ili ikue, lazima sekta binafsi nayo iendelee kukua. Nichukue fursa hii, Mhe. Makamu wa Rais, kukushukuru sana, kwa jitihada kubwa ambazo zinafanywa na Serikali yetu ya awamu ya sita, chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, za kuchochlea maendeleo ya sekta ya fedha na ukuaji wa uchumi nchini.

Uwepo wako hapa katika mukutano huu, unadhihirisha vipaumbele vyta Serikali katika kuweka mazingira wezeshi ya kuimarisha ukuaji wa uchumi, ikiwemo sekta ya fedha, hasa nyakati hizi zenye changamoto za kiuchumi, ikiwa ni pamoja na kuweka sera nzuri na ushirikishaji zitakazofanya sekta binafsi ikue kwa haraka.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, ninaomba nitumie fursa hii kuwakaribisha tena wageni wote kwenye mkoa wetu wa Arusha ambao ni kivutio cha utalii nchini; muweze kujiona na kufurahia vivutio mbalimbali vilivyopo katika mkoa wetu, ikiwa ni pamoja na hifadhi za taifa, na hasa Hifadhi ya Taifa ya Arusha, ambayo inapatikana kilometa chache kutoka jiji hili la Arusha; Hifadhi ya Ngorongoro ambayo ni sehemu ya urithi wa dunia, Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, Mlima Meru, Mlima Oldonyo Lengai, pia muweze kujiona mazingira mazuri, na kilimo cha bustani na matunda kwenye wilaya yetu hasa ya Arumeru, lakini pia uoto wa asili, hoteli za kitalii, pamoja na kufurahia ukarimu wa wana Arusha.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, tunakutakia kila la heri katika majukumu yako makubwa yaliyo mbele yako, ya kuendelea kuwahudumia Watanzania. Pia, tunakushukuru tena kwa kutenga muda wako na kuja kututembelea wana Arusha na kushiriki katika mukutano huu mkubwa.



Ninawatakiwa washiriki wote wa mkutano huu kila la heri na Mwenyezi Mungu aendeleee kubariki nchi yetu.

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

1.3 Salamu kutoka kwa Bw. Theobald Sabi, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mabenki Tanzania

Mhe. Dkt. Philip Isidor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Mhe. Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha;

Mhe. Emmanuel Mtatifikolo Kaganda, Mkuu wa Wilaya ya Arumeru,

Mhe. Emmanuel Tutuba, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania;

Manaibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania;

Mabibi na Mabwana;

Itifaki imezingatiwa.

Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

Mheshimiwa Makamu wa Rais, Wageni waalikwa,

Kwa niaba ya jumuiya ya Mabenki Tanzania, napenda kumshukuru Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia kukutana hapa, siku hii ya leo. Kongamano hili ni muhimu sana kwetu kwenye sekta ya fedha na hivyo uwepo wako hapa unatupa faraja kubwa sana, Mhe. Makamu wa Rais, asante sana.

Mada kuu ya kongamano hili la 21 ni: Kuimarisha ustahimilivu wa sekta ya fedha nyakati za changamoto za kiuchumi. Hali ngumu ya uchumi duniani kwa sasa inayotokana na kupanda kwa riba kwenye masoko ya fedha duniani, vita inayoendelea kati ya Ukraine na Urusi inayotishia kuendelea kupanda kwa bei za bidhaa mbalimbali kama vile petrol and diseli, madhara yaliyotokana na janga la UVIKO-19, na changamoto zingine zikiwemo mabadiliko ya tabianchi na uhalifu wa kimtandao, yaani 'cyber crime', imeendelea kuathiri sekta ya fedha hapa nchini.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, ni wazi kwamba changamoto hizi zitaendelea kuwepo duniani lakini kama wanavyosema wahenga, bahari tulivu haimpimi nahodha wa meli, ni katika nyakati kama hizi ambapo sisi tulioko kwenye sekta ya fedha tunapaswa kuja na majibu. Hivyo basi, wakati ambapo sekta ya fedha duniani inapitia majoribu haya, kwetu ni muda sahihi wa kukutana kuchangia mawazo ili kwa pamoja tuweze



kubuni mbinu za kukabiliana na changamoto hizi. Hivyo, kupata fursa ya kuwa nawe kwenye kongamano hili, ni jambo la kutia moyo sana kwenye sekta ya fedha. Asante sana Mhe. Makamu wa Rais.

Mwelekeo wetu kwenye Umoja wa Mabenki ni kuendelea kukabiliana na changamoto hizi ili kupunguza athari za majanga na hivyo kuziwezesha sekta muhimu kama vile kilimo, viwanda, utalii, na wajasiriamali wadogo wadogo kuendelea kustawi. Jukumu letu katika kuwezesha wananchi kiuchumi tunaangalia kulitekeleza na tunajivunia ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi, ongezeko ambalo kufikia Desemba 2023, lilifika asilimia 17.1.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, mabenki yanaendelea kuwa sehemu muhimu ya sekta ya fedha hapa nchini na tukirudi nyuma tukaangalia wakati wa janga la UVIKO-19, mabenki nchini kwa ujumla yalichukua hatua za makusudi kuweka masharti yaliyokuwa rafiki ili kuwawezesha wakopaji na wananchi walioathirika kwa ujumla, hasa kwenye sekta ya utalii, malazi na usafirishaji, kuweza kumudu kipindi kile kigumu. Ni imani na nia yetu kwenye sekta ya fedha kwamba, pale ambapo patatokea hali ngumu mabenki yatakuwa tayari kuchukua hatua stahiki ili kuhakikisha kwamba sekta zetu za uzalishaji zinaendelea kupata uwezo unaohitajika.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, benki zinaendelea kuchukua hatua kuongeza wigo wa upatikanaj wa huduma jumuishi za kifedha kwa wananchi walio wengi ama financial inclusion. Ripoti ya Finscope ya mwaka 2023 inaonesha huduma jumuishi za fedha kwenye sekta ya kibenki ilikuwa asilimia 22, ikiwa imeongezeka kutoka asilimia 17 kutoka mwaka 2017. Ongezeko hili ni matokeo ya juhudhi mbalimbali za makusudi za Serikali, Benki Kuu ya Tanzania na mabenki hapa nchini. Tunakubali ujumuishi wa asilimia 22 bado ni mdogo na hivyo kuna haja ya kuelekeza nguvu kuongeza ujumuishi huu.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, mabenki yanaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu ufahamu juu ya fursa za kifedha hasa mikopo, ili wananchi wengi zaidi waweze kufaidika na huduma rasmi za mikopo na hivyo kushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi nchini.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, naomba nimalizie kwa niaba ya Umoja wa Mabenki hapa nchini, kuishukuru Serikali chini ya Rais wetu Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuweka mazingira bora ya kiuchumi yanayopelekea mabenki kuendelea kukua, kuimarika na kuwafikia Watanzania wengi zaidi. Shukrani za kipekee tunazielekeza kwa Wizara ya Fedha, Benki Kuu ya Tanzania na wasimamizi wengine wa sekta ya fedha kwa kuendelea kutupa miongozo na kujenga mazingira rafiki kati ya wasimamizi na mabenki.



Tunaahidi, Mhe. Makamu wa Rais, kuendelea kusimama kama mhimili muhimu sana katika kufikia malengo ya kitaifa ya ujenzi wa uchumi shirikishi. Na kama nilivyo sema hapo awali, changamoto hazitaisha, zitaendelea kuwepo, nyingi zikiwa ni changamoto za kidunia na sisi, sekta ya kifedha, tutaendelea kutafuta masuluhi shio yanayoendana na mazingira yetu hapa nchini.

Asante sana kwa kunisikiliza.

1.4 Maneno ya Utangulizi kutoka kwa Bw. Emmanuel Tutuba, Gavana, Benki Kuu ya Tanzania

Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Viongozi wote mliopo meza Kuu;

Wageni wote waalikwa;

Mabibi na Mabwana;

Itifaki imezingatiwa.

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

Mheshimiwa Makamu wa Rais, awali ya yote naomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na utukufu, ambaye kwa namna ya pekee ametuwezesha kusafiri na kukutana mahali hapa kwa ajili ya kongamano la 21 la Taasisi za Fedha, maarufu kama *Conference of Financial Institutions*, au 21st COFI. Kwenye mkutano huu, tumefanikiwa kuwa na washiriki takribani 1,000, ambapo washiriki 43 wamethibitisha kushiriki kwa njia ya mtandao. Kwa hiyo, ni mkutano mseto (hybrid meeting).

Mheshimiwa Makamu wa Rais, pia naomba kutumia fursa hii kwa heshima na taadhima, kuwakaribisha nyote kwenye kongamano hili ambalo hufanyika kila baada ya miaka miwili. Kongamano hili linatoa fursa kwa wadau wote muhimu wa sekta ya fedha kubadilishana mawazo na uzoefu kuhusu mafanikio, changamoto na mikakati inayoweza kutekelezeka katika kuongeza ufanisi na tija na kuleta maendeleo ya sekta ya fedha na uchumi. Tangu tulipofanya kongamano la 20 jijini Dodoma, mwaka wa fedha 2021/22, sekta ya fedha imeendelea kutekeleza maboresho mengi ya kimfumo, kumuundo na kiutawala, hali iliyowezesha sekta hii kuendelea kukua kwa kasi na kuongeza mchango wake katika ukuaji wa uchumi.



Mheshimiwa Makamu wa Rais, napenda pia kukushukuru wewe binafsi kwa kutenga muda wako ili kuhudhuria na kufungua kongamano hili muhimu la mwaka 2024. Uwepo wako hapa leo unadhihirisha umuhimu mkubwa unaotolewa na Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kusimamia maendeleo ya sekta ya fedha nchini. Pia, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wa Fedha pamoja na Naibu Waziri wa Fedha, Makatibu Wakuu na manaibu wao wa wizara zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa namna ambavyo wamekuwa wakitupatia ushirikiano mzuri katika kufanikisha majukumu yetu ya kusimamia sekta hii kwa ujumla.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, vile vile namshukuru Mhe. Mkuu wa Mkoa, John Mongella ambaye naye tumekuwa tukishirikiana vema, pia nishukuru uwepo wa mwakilishi wake, Mhe. Emmanuel Kaganda, pamoja na wakuu wa wilaya wote na sekretariati ya mkoa kwa ushirikiano waliotupatia katika maandalizi ya kongamano hili. Naomba pia niwashukuru watoa mada wote ambao wameweza kujianaa kwa ajili ya kuja kushiriki kongamano hili.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, kama ulivyonuelekeza mara ya mwisho kwamba tuendelee pia kutangaza lugha yetu ya Kiswahili, kongamano hili litatumia lugha ya Kiswahili na kiingereza. Aidha, tumeandaa utaratibu wa tafsiri (interpretation) kwa ajili ya waalikwa waliotoka nje ya nchi ikiwemo Uingereza, Marekani, Zimbabwe, Bangladesh, Nigeria, na wageni wengine wasiojua lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, naomba niendelee kuwashukuru washiriki wote ambao wameweza kufika hapa. Kutokana na umuhimu wa kongamano hili ninaamini tutapata fursa ya kuendelea kujadiliana masuala mengi zaidi.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, kama alivyosema Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mabenki, mada kuu ya kongamano hili la 21 ni "Kuimarisha Ustahimilivu wa Sekta ya Fedha Nyakati za Changamoto za Kiuchumi". Mada hii imechaguliwa kwa kuzingatia mazingira ya sasa ya Kiuchumi na changamoto zilizotokana na janga la UVIKO-19, migogoro ya kisiasa katika baadhi ya nchi duniani, athari za mabadiliko ya tabianchi na kutotabirika kwa sera za fedha katika baadhi ya nchi zenye uchumi mkubwa duniani. Changamoto hizi zimesababisha, pamoja na mambo mengine, kuwepo kwa athari hasi katika mnyororo wa usambazaji na ongezeko la bei za bidhaa na huduma duniani; na kuwepo kwa hali ngumu ya upatikanaji wa fedha katika masoko ya ndani na nje; na kushuka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia. Katika mazingira kama haya, ni muhimu kuwa na sekta ya fedha iliyoi mara na madhubuti zaidi, ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa mifumo thabitii inayoendana na wakati wa sasa. Uwezo wa



taasisi za kifedha na utayari wa kukabiliana na changamoto wakati wote ni muhimu ili kuleta uhimilivu na ustahimilivu wa uchumi, pamoja na kudumisha ustawi wa jamii na wa kisiasa nchini.

Katika kujadili mada kuu niliyoitaja hapo juu, washiriki wa kongamano hili watapata pia fursa ya kusikiliza mawasilisho yaliyoandaliwa na watoa mada katika maeneo makubwa matatu:

- i. **Ufanisi na uhimilivu wa taasisi za fedha wakati wa majanga:** Katika mada hii, nafahamu kwamba, wakati wa majanga au mikasa mbalimbali, taasisi za fedha zinakutana na changamoto mbalimbali, zikiwemo ongezeko la mikopo chechefu (isiyolipika), kupungua kwa mitaji na kuongezeka kwa gharama za fedha za mikopo n.k. Majadiliano chini ya mada hii yanatarajiwa kutoa mwanga kuhusu namna taasisi za fedha zinavyoweza kujikwamua na athari zinazotokana na majanga hayo, pamoja na kupata uzoefu wa hivi karibuni jinsi taasisi hizo zinavyopaswa kujiweka tayari katika kukabiliana na kujikinga na athari za majanga yanayoweza kujitokeza hapo baadaye.
- ii. **Uhimilivu wa sekta ya fedha katika kukabiliana na changamoto za kiuchumi: Sheria mbalimbali, ubunifu na usimamizi wa vihatarishi.** Mada hii itabainisha changamoto za hivi karibuni duniani, ubunifu na mabadiliko katika mifumo ya usimamizi wa vihatarishi kwa pamoja, na madhara yanayoweza kujitokeza. Mada hii, pia itaangazia marekebisho katika mifumo ya udhibiti ili kuhakikisha ustahimilivu wa sekta ya fedha. Majadiliano kwenye eneo hili yanatarajiwa kujikita zaidi katika masuala ya ufanisi wa sheria na kanuni mbalimbali za kifedha, njia za ubunifu na mikakati imara inayoweza kuimarisha usimamizi wa vihatarishi katika ustahimilivu wa sekta ya fedha.
- iii. **Ubunifu wa kiteknolojia katika utoaji wa huduma za kifedha: Kichocheo cha ustahimilivu.** Mada hii itabainisha ubunifu wa teknolojia mpya unavyotoa fursa kwa taasisi za fedha katika kuboresha utoaji wa huduma za kifedha na namna ya kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazoweza kujitokeza kutokana na teknolojia hizo. Mada hili inatarajiwa kuongeza ufahamu zaidi kuhusu jinsi ya kutumia maendeleo ya teknolojia ili kujenga sekta imara ya fedha.

Tunashukuru kwa dhati watoa mada wote ambao tumewaalika kutoka ndani ya nchi, na wale waliotoka Zimbabwe, Kenya, Marekani, Bangladesh, Uingereza na Nigeria ambao kwa umahiri wao, naamini, watazitendea haki mada hizo na wachangiaji pia watapata fursa ya kutoa mawazo yao na baadaye watakuja na mikakati ambayo naamini tutaitumia katika kuimarisha sekta yetu ya fedha hapa nchini.



Mheshimiwa Makamu wa Rais, licha ya changamoto za kiuchumi duniani, bado uchumi wa Tanzania umeendelea kukua kwa wastani wa asilimia 4.8 katika kipindi cha mwaka 2020 na 2022, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.3 ya ukuaji wa uchumi katika nchi za Afrika zilizopo kusini mwa Jangwa la Sahara katika kipindi hicho. Aidha, kati ya mwaka 2020 na 2023, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.8, ambao uko chini ya asilimia 5, ambalo ni lengo tulilojiwekea kama nchi kwa kipindi cha kati. Hali hii ilisababishwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti, pamoja na mageuzi makubwa ya kimuundo yanayoendelea nchini.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, kama sehemu ya kuimarisha ufanisi wa sera ya fedha na kuendana na Itifaki ya Umoja wa Fedha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambayo inalenga kuwa na sarafu moja katika ukanda wetu wa Afrika Mashariki ifikapo mwaka 2031, mwezi Januari 2024, Benki Kuu ya Tanzania ilihama rasmi kutoka katika mfumo wa sera ya fedha unaotumia ujazi wa fedha na kuanza rasmi kutumia mfumo mpya unaotumia riba. Hii inamaanisha kwamba katika kutekeleza sera ya fedha, Benki Kuu sasa itakuwa ikitangaza riba yaani *Central Bank Rate - CBR* ambayo itakuwa inatoa mwelekeo wa sera ya fedha katika kipindi cha robo mwaka. Tayari kuanzia mwezi Januari 2024 nilitangaza riba elekezi ya asilimia 5.5 ikiwa na wigo wa asilimia 2 kwenda juu au kushuka chini. Riba hii imeendelea kuzingatiwa katika robo ya mwaka huu na tumeona inaendelea vizuri na niwashukuru watendaji wakuu wote wa mabenki ambao ninawaona hapa ambao wameendelea kuzingatia maelekezo yangu wakati naitangaza riba hiyo. Ni matarajio yangu kwamba benki na taasisi nyingine za fedha zitatumia kiwango cha riba ya Benki Kuu kama kiashiria muhimu cha mabadiliko ya viwango vya riba kwa wateja wa taasisi hizo nchini na wateja wengine wanaopata mikopo kutoka kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, pamoja na athari za mitikisiko mbalimbali ya uchumi duniani, sekta ya fedha ya Tanzania imebaki himilivu na imeendelea kuwa mionganoni mwa sekta zinazokua kwa kasi hasa baada ya janga la UVIKO-19. Aidha, sekta hii imeendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa sera ya fedha na kurahisisha malipo hapa nchini. Katika mwaka 2022, sekta hii ilikua kwa asilimia 9.2 na kuchangia ukuaji wa Pato la Taifa kwa asilimia 6.6. Ukuaji huu ulikuwa bora ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.1 na mchango wa asilimia 2.2 kwenye ukuaji wa Pato la Taifa mwaka 2020.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, sekta ya fedha imekuwa na ongezeko la huduma mpya za kifedha na mabadiliko ya mifumo ya utoaji wa huduma, ikisaidiwa na uvumbuzi na mabadiliko ya teknolojia. Hadi sasa, miamala mbalimbali kama vile uhamishaji wa fedha, malipo ya ankara na kodi, pamoja na huduma nyingine inafanyika muda



mfupi kupitia mifumo ya kidigitali. Hapo awali tunakumbuka kwamba miamala ya fedha ilikuwa ikifanyika nje ya mifumo ya kidigitali ambapo watu wengine walikuwa wanatumia makaratasi na wengine kusafirisha fedha kwenye vifurushi kutoka kituo kimoja kwenda kingine na hivyo kuchukua muda mrefu, hatari ya kupotea na kuwa na gharama kubwa. Kwa sasa, Serikali imeweka mazingira wezeshi kwa wadau mbalimbali kutumia ubunifu katika mifumo ya kidigitali na mitandao ya mawasiliano kufanya miamala ya fedha kwa urahisi. Aidha, wadau wa sekta ya fedha wanaendelea kuboresha matumizi ya mifumo ya kidigitali na kurahisisha uhaulishaji wa miamala ya kifedha. Mfano mzuri, huduma za malipo kwa njia ya simu za mkononi ambazo zimeendelea kuongezeka na kuboresha uhimilivu wa sekta ya fedha na uchumi dhidi ya majanga yanayojitokeza hapa nchini.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, pamoja na shughuli nyingine za kongamano hili, leo Benki Kuu ya Tanzania itazindua Mfumo wa Taifa wa Malipo ya Papo kwa Papo, yaani Tanzania Instant Payment System (TIPS). Uzinduzi wa mfumo huu unathibitisha dhamira ya Serikali ya awamu ya sita ya kutumia ipasavyo mifumo ya kidigitali katika kurahisiah mazingira mazuri ya biashara, kuongeza ufanisi katika utendaji kazi, na kupunguza gharama na muda katika kufanya malipo. Katika kutekeleza azma hiyo, Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kusimamia mifumo ya malipo kwa wadau mbalimbali na kudhibiti vihatarishi mbalimbali vinavyoweza kujitokeza kupitia mifumo ya malipo. Aidha, Benki Kuu imeweza kufanya ubunifu kwa kutengeneza mfumo huu wa TIPS kwa kuzingatia viwango vya kimataifa. Mfumo huu unakuja wakati ambapo unahitajika sana ili kurahisisha zaidi shughuli za kifedha nchini, na tunaamini kwamba utakidhi viwango na matarajio ya wananchi kwa kuwa umeshirikisha wadau wote muhimu katika kuunda.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, mchakato wa kuanzisha TIPS ulifanywa na Benki Kuu ya Tanzania kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru sana wadau walioshiriki katika kuunda mfumo huu. Kwanza ni Ofisi ya Rais, pili ni Wizara ya Fedha, tatu Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, nne Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, tano Mamlaka ya Mapato Tanzania, sita Mamlaka ya Serikali Mtandao, saba Financial Sector Deepening Trust (FSDT) na nane ni Bill and Melinda Gates Foundation.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, majoribio ya mfumo huu yalianza mwezi Agosti 2022 kwa kuunganisha benki tatu na kampuni mbili za mawasiliano ya simu. Hadi sasa mfumo huu wa TIPS umeunganishwa kwenye benki zote na makampuni yote yanayotoa huduma za fedha mtandaoni. Kwa sasa, TIPS inawezesha miamala inayohusisha taasisi na mitandao mbalimbali (interoperable transfers). Kwa kutumia mfumo huu, miamala inaweza kufanyika Mtu kwa Mtu (Person to Person - P2P),



Mtu kwa Biashara (Person to Business - P2B), na Mtu kwa Wafanyabiashara (Person to Merchants - P2M). Pia, teknolojia ya “QR code” imeanza kwa majaribio kufikisha miamala toka kwa mlipaji kwenda kwa mtu anayepokea fedha. Mipango ya hivi karibuni ni kuunganisha TIPS na mfumo wa malipo wa Serikali wa GePG ili kurahisisha uhaulishaji wa fedha na malipo ya Serikali.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, ni matarajio yetu kwamba matumizi ya TIPS yataongeza upatikanaji wa huduma za kifedha za kidigitali na kupunguza matumizi ya fedha taslimu nchini, sambamba na utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Kifedha (2023-2028), lakini pia kuendana na Mpango Mkuu wa Maendeleo ya sekta ya fedha (2020/21 - 2029/30) wenye lengo la kukuza huduma za kifedha za kidigitali ili kufikia uchumi usiotumia fedha taslimu. Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kuhakikisha panakuwepo utulivu wa bei na ustahimilivu katika sekta ya fedha kwa kuweka mazingira rafiki ya usimamizi na udhibiti wa mifumo ya malipo nchini.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, nichukue fursa hii tena kuzishukuru Serikali zetu zote mbili yaani Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa namna ambavyo tumeendelea kushirikiana kutekeleza majukumu haya. Aidha, niwapongeza Jumuiya ya Mabenki Tanzania (TBA), pamoja na taasisi zote zilizoshiriki kuandaa m Kutano huu, lakini pia katia utekelezaji wa majukumu waliyokasimiwa.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, naomba nimalize maelezo yangu kwa kurudia tena kukushukuru wewe binafsi kwa kuja kushiriki nasi katika tukio hili. Niendelee kuwashukuru wote kwa ushiriki wenu. Na sasa, kwa ridhaa yako naomba kuonyesha kipande cha makala (video clip) kinachotoa ujumbe mahsus wa mfumo wa TIPS ambao utauzindua hivi punde.

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

1.5 Salamu za Ukaribisho kutoka kwa Mhe. Hamad H. Chande, Naibu Waziri wa Fedha

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Dkt Philip Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini;

Mheshimiwa Emmanuela Kaganda, Mkoo wa Wilaya ya Arumeru na Mwakilishi wa Mkoo wa Mkoa wa Arusha;

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Arusha;



Waheshimiwa Wabunge wote mliopo, wakiwemo Wenyeviti wa Kamati za Bajeti, PAC na PIC;

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya Wote Mliopo;

Makatibu Wakuu Wote Mliopo;

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania;

Itifaki imezingatiwa

“Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania”

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, ninayo heshima kubwa kukualika katika kongamano la 21 la Taasisi za Fedha nchini. Nakushukuru kwa kutenga muda wako kuja kuungana nasi leo katika tukio hili muhimu sana, si tu la kongamano lakini pia la uzinduzi wa TIPS. Uwepo wako hapa leo ni ushuhuda wa thamani kubwa unayoipa sekta ya fedha katika ajenda ya maendeleo. Nampongeza Mheshimiwa Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bwana Emmanuel Tutuba, na Jumuiya ya Mabenki Tanzania kwa kuandaa tukio hili muhimu. Pia nawashukuru nyote mliohudhuria kwa kutoa muda wenu kwa ajili ya Kongamano hili.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, uandaaji wa kongamano hili umefanyika katika muda sahihi, ukizingatia mabadiliko yanayoendelea na changamoto kubwa zinazotokana na mitikisiko ya kiuchumi duniani. Katika nyakati kama hizi, ushirikiano wa karibu baina ya wadau wa sekta ya fedha ni muhimu ili kuhakikisha uimara wa sekta ya fedha. Hii inajumuisha kwa kiasi kikubwa kuwa na sera sahihi, mfumo wa kisheria na mfumo wa udhibiti.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, mada kuu iliyochaguliwa katika kongamano hili: “Kuimarisha Ustahimilivu wa Sekta ya Fedha Nyakati za Changamoto za Kiuchumi”, inakwenda sambamba na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025, inayojikita katika kujenga uchumi imara, thabiti na wenyewe ushindani, uwezo wa kuhimili changamoto mbalimbali na kubadilika kulingana na mazingira yaliyopo. Maazimio yatakayopatikana kutokana katika kongamano hili yatasaidia kutoa mwanga juu ya mafanikio tuliyoyapata kwa juhudi zetu na kutuongoza kuendelea kujenga uchumi shirikishi na endelevu.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Serikali kuititia Wizara ya Fedha imekuwa ikitekeleza jukumu muhimu katika juhudi za kuimarisha sekta ya fedha kulingana na Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha 2020/21 - 2029/30. Wizara ikiwa msimamizi wa sera za kiuchumi, inashirikiana kwa karibu na wadau wa sekta ya fedha kutekeleza hatua zinazosaidia kuimarisha seka ya fedha kwa kutunga na kutekeleza sera zinazoboresha mazingira ya udhibiti, kuimarisha mfumo wa usimamizi wa vihatarishi,



na kukuza uwezo ndani ya sekta ya fedha.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, kama alivyosema Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, sekta ya fedha ya Tanzania imeonyesha uhimilivu katika kupambana na changamoto za uchumi wa dunia za hivi karibuni. Uimara wa mabenki umesaidiwa na uwiano mzuri wa mtaji na ukwasi ambao ulikuwa juu ya mahitaji ya chini ya udhibiti. Ufanisi huo unajionyesha katika ukuaji wa rasilimali (assets), hasa mikopo kwa sekta binafsi, ambayo ilikua kutokana na teknolojia za kifedha za hali ya juu na hatua zilizochukuliwa na Serikali na Benki Kuu ya Tanzania kuimarisha uchumi.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, mikopo hatarishi pia imebakia katika viwango vya chini, kama inavyoonekana kwenye kupungua kwa mikopo chechefu ambayo ipo chini ya kikomo cha asilimia 5 ya mikopo yote. Aidha, ongezeko la faida katika sekta ya benki limeongeza uimara wa kuhimili changamoto mbalimbali katika sekta hii.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, masoko ya fedha na mitaji yalibaki kuwa imara na thabiti, na hivyo kuongeza ushiriki wa wawekezaji wa ndani. Sekta ya bima pia iliweza kuhimili changamoto kwa kuwa na mtaji na ukwasi wa kutosha kama inavyojionyesha kwenye ongezeko la malipo kamili na faida. Ufanisi huu mzuri pia ulionekana katika sekta ya hifadhi ya jamii, ambayo ilikuwa imara, kwa kuongezeka kwa mali na uwezo wa kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, kuhusu huduma jumuishi za fedha, tumeshuhudia mafanikio makubwa hasa kwenye ongezeko la upatikanaji na utumiaji wa huduma rasmi za kifedha kama ilivyoonyeshwa kwenye matokeo ya utafiti wa FinScope wa mwaka 2023. Utafiti huu ulionyesha kuwa upatikanaji wa huduma rasmi za kifedha nchini uliongezeka kutoka asilimia 86 mwaka 2017 hadi asilimia 89 mwaka 2023. Pia utafiti ulionyesha matumizi ya huduma rasmi za kifedha yaliongezeka kutoka asilimia 65 hadi asilimia 76 . Mafanikio haya kwa kiasi kikubwa yalichangiwa na uwepo wa huduma za kifedha kwa njia za kidigitali, kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu bidhaa na huduma za kifedha zinazotolewa na taasisi za fedha nchini, na ushirikiano imara kati ya wadau wa sekta ya fedha. Wizara inakusudia kuendelea kushughulikia masuala yanayohusiana na elimu ya kifedha na ubora wa huduma za kifedha nchini, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wake kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, ninaamini kwamba, hekima, uzoefu wetu, na utayari wetu wa kujitoa unahitajika ili kuimarisha mfumo wa kifedha nchini ili uwe wenye nguvu na imara zaidi. Tunashukuru tumpata watoa mada mahiri na wenye weledi kutoka ndani na nje ya nchi ambao wapo tayari kutupatia uzoefu wao.



Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika mapinduzi ya malipo ya huduma na bidhaa kwa kutumia simu za mikononi na benki za kidigitali. Tayari mamilioni ya Watanzania wananaufaika na upatikanaji wa huduma za kifedha zinazotolewa kwa njia ya simu. Kuongezeka kwa huduma za kifedha zinazotolewa kwa njia ya simu kumeboresha kwa kiasi kikubwa namna ya kufanya na kutuma miamala ya kifedha, hivyo kuwawezesha wananchi na wafanyabiashara kusimamia fedha zao kirahisi na usalama zaidi.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, napenda kumpongeza Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania na taasisi washirika kwa kuunda Mfumo wa Malipo ya Papo kwa Papo (TIPS) ambao utauzindua leo. Kama ilivyoelezwa na Gavana, mfumo huu utawezesha uhamishaji wa fedha papo kwa papo kati ya watoa huduma mbalimbali wa mifumo ya malipo, ikijumuisha benki na watoa huduma wa pesa kwa njia ya simu na njia nyingine za kielektroniki. Inategemewa mfumo huu utasaidia kupunguza gharama za uendeshaji kwa watoa huduma na gharama za miamala kwa watumiaji.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, nichukue fursa hii tena kukushukuru, kwa niaba ya sekta ya fedha nchini na wadau wengine, kwa kukubali mwaliko wetu wa kufungua rasmi kongamano la 21 la Taasisi za Fedha na kuzindua Mfumo wa Malipo ya Papo kwa Papo (TIPS). Tunapenda kukuhakikisha kwamba tutatoa ushirikiano wetu katika juhudzi za Serikali za kuboresha maisha ya Watanzania na kuifanya Tanzania kung'ara katika jukwaa la kimataifa.

Baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Makamu wa Rais, ninayo heshima kubwa kukualika rasmi kufungua kongamano la 21 la Taasisi za Fedha na kuzindua Mfumo wa Malipo wa Papo kwa Papo (TIPS).

Mheshimiwa Makamu wa Rais, karibu sana!

Asante Sana!

1.6 Hotuba ya Ufunguzi ya Mgeni Rasmi, Mhe. Dkt. Philip I. Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mheshimiwa Hamad Chande, Naibu Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini;

Mheshimiwa Emmanuel Kaganda, Mkoo wa Wilaya ya Arumeru na Mwakilishi wa Mkoo wa Mkoa wa Arusha;



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Arusha;

Waheshimiwa Wabunge wote mliopo, wakiwemo Wenyeviti wa Kamati za Bajeti, PAC na PIC;

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya Wote Mliopo;

Makatibu Wakuu Wote Mliopo;

Waheshimiwa Mabalозi na Viongozi Wawakilishi wa Mashirika ya Maendeleo Mliopo;

Wakurugenzi wa Bodi ya Benki Kuu ya Tanzania;

Gavana Wa Benki Kuu ya Tanzania;

Manaibu Gavana wa Benki Kuu;

Magavana Wastaafu wa Benki Kuu Mliopo;

